# Tazama mzabibu wako Bwana

**Zaburi 79** 9,10, 1314, 15 16, 19 20

Gloire VINCENT




1. Ulingoa mzabibu toka Misri,
ukawafukuza mataifa, ukaupanda;
kwake ukapalia udongo, tayari,
nao ukatoa mizizi, ukaijaza nchi.

2. Kwa nini umebomoa kuta zake,
ili wote wanaopita njiani wachume zabibu zake?
Ili nguruwe wa mwituni auharibu,
na wanyama wa porini wautafune?

3. Ee Mungu wa majeshi, urudi,
uangalie toka mbinguni, uone,
uje kuutazama mzabibu huo.
Uulinde huo uliopanda kwa mkono wako wa kuume,

4. Hatutakuacha tena hata kidogo;
utatutunzia maisha, nasi tutaomba jina lako.
Ee Bwana, Mungu wa majeshi, utusimike tena,
uangazishe uso wako,nasi tutaokoka.